





Mhubiri wa Kimataifa lameck Lister nilizaliwa mnamo mwaka 1986 tarehe 08 Mwezi wa nane Morogoro Tanzania. Nilikoka nikiwa kidato cha tatu mwezi kati ya wa saba na wa nane 2003 shule ya sekondari kibaha mkoa wa Pwani.

Yesu alikufa kw ajili ya wenye dhambi wote apate kuwaokoa kutoka ktk maisha ya dhambi na madhara yake na amefufuka yuko hai ampe ampokeaye kw moyo maisha yake yaani maisha mapya yenye mpango na kusudi la mungu

Alinitokea kibaha sekondari ktk miaka 2005 - 2007. Mimi nashuhudia kuwa amefufuka kwa kuwa nimemuona. Ukiwa unaamini nisemayo nenda kaokoke.

CONTACT : MH. WA KIMATAIFA MINISTRY.

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM - TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

FAX: +25522 222772579 (EFATHA)

TEL: +255 22 2773535 (EFATHA)







# MHUBIRI WA KIMATAIFA

# MHUBIRI


# WA

# KIMATAIFA

Mhubiri wa kimataifa ni mtumishi wa Yesu aliyeitwa na Yesu kuwahubiri wenye dhambi (Kimataifa) waokoke.

(watubu + wabatizwe kwa maji mengi + kujazwa roho mtakatifu)

kwa jina la Yesu kwa kumwamini Yesu na kumfuata siku zote za maisha yao ya ubatili waliyopewa chini jua.




**Na Mhubiri wa Kimataifa**

**<u>Lameck Lister</u>**

TANGAZO

<u>Mhubiri wa injili;</u>

**"Usikengeuke ktk huduma ya kuhubiri kwa saba-bu ya hekima";**

Epuka kuwa mwalimu wa kanisa au mchungaji wa kani-sa.Ikiwa Yesu amekuita akakupa huduma moja tu ya mhubiri hata kama akiukupa hekima kama mhubiri Filipo.

YESU NI MFALME

BWANA NA MWOKOZI

## MAWASILIANO

Sasa umeokoka unaweza kwenda kwa huduma au kanisa la watu waliokoka utawatambuaje kwa ishara zilizoandikwa ktk Marko 16:16 kuanzia viongozi wao wahuduma au kanisa hadi washirika au waamini au watumishi.

Ukiwa na uhitaji wowote waweza wasiliana nasi kupitia barua pepe :

**listerlameck5@gmail.com,+255658601034,Efatha church;P.o Box 356666;Mwenge –DSM**.

Yesu wangu na Bwana wangu akubariki asikupungukie kwa elimu, kazi, mke au mume mzuri na watoto,makazi mazuri, furaha, amani na upendo wake wa kukuwezesha kumpenda yeye na kanisa lake. Amen

## CONTACT

MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY.

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM

TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

FAX: +25522 222772579 (EFATHA)

TEL: +255 22 2773535 (EFATHA)

© MHUBIRIWA KIMATAIFA MINISTRY, FIRST EDITION 2023

ISBN: 1986 - 08 - 08 - 01

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiruhusiwi kunakili, kutafsiri au kuchapisha kwa njia yoyote bila ruhusa ya Mhubiri wa Kimataifa ministry au Mhubiri wa Kimataifa Lameck Lister. Nakuu zote zimetoka ktk biblia (Maandiko matakatifu in Swahili Union Version)

## SHUKRANI

Namshukuru Yesu kwa kuniwezesha kutoa toleo hili la kwanza la kitabu cha MHUBIRWA KIMATAIFA. Kitabu hiki namtolea Yesu na Baba yake mapenzi yake yatimie kwa walioitwa na Yesu kuwa wahubiri. Awanurukishie akili zao zipate uelewa au ufahamu juu ya kusudi lake ktk maisha yao. Asante Baba wa Yesu na Yesu pia. Amen.

## YALIYOMO


1. UTANGULIZI
2. WITO
3. HEKIMA
4. UPONYAJI
5. MIUJIZA
6. KUPOZA
7. AMRI YA KUTOA PEPO
8. BARAKA
9. MKE
10. ELIMU
11. KUMWONA YESU
12. MALAIKA
13. KUOKOKA
14. USHAURI WA AJABU
15. MHUBIRI WA KIMATAIFA
16. UPONYAJI WA JASHO LA KWAPA
17. KUMWONA MUNGU
18. MWISHO


SALA YA KUOKOKA

Mwinjilisti kwa kufanya hivyo. Huduma zote mbili Mtume Paulo anazisema ya mhubiri na mwinjili. Tafakari kwa nini mtume Paulo aangike hivi ktk nyaraka zake.**“ ..injili ni uweza uletao wokovu...” (Rum 1:16);**

**“Naye alitoa wengine kuwa...wainjilisti..”(waef 4:11);**

Ukiwa umesoma kitabu hiki na umeguswa wito wa kuokoka kwangu na sehemu zingine za kitabu sasa unaka kubadilisha maisha yako kwa kuachana na dhambi kuokoka na kumfuata Yesu siku zote za maisha yako kwa kumtumikia kama bwana na mwokozi fuatisha sala hii**.**

**“Bwana Yesu nakubali mimi ni mwenye dhambi naamini wewe ni Bwana uliyesulubiwa kwa ajili ya dhambi zangu zipate kusamehewa na kuondolewa kwa damu yako iliyomwagika msalabani,Bwana yesu nisamehe na kuniondolea dhambi zangu nilizofanya toka tumboni mwa mama yangu. Asante Bwana Yesu kwa kunisamehe na kuniondolea dhambi zangu .Bwana Yesu naamini Mungu alikufufua ktk wafu siku tatu baada ya kusulubiwa ili nipewe haki ya maisha yako ,Bwana Yesu karibu ndani ya moyo wangu nijaze roho wako mtakatifu”**. Amen

## SURA YA THELATHINI NA SITA

MWISHO

Asante Yesu na Baba yake kwa kunifanikisha kuandika kitabu hiki chenye Jina la **“Mhubiri wa kimataifa”** chenye kusudi la kumfahamisha mhubiri wa injili; uwe **Mhubiri wa kimataifa**, **Mhubiri wa mataifa** au **mhubiri** (kwa taifa: jifunze kwa mhubiri Filipo **matendo 8:13 ,8:39-40,21:8**

Sehemu kubwa alihubiri injili ndani ya nchi ya Israel hata mikutano ya injili pia) **kusudi la Yesu** akutumie kuokoa wenye dhambi wengi sana kutoka ktk maisha ya dhambi na madhara yake kwa kukupeleka uwahubiri injili yake wapate **kuokoka.**

Lakini pia kitabu hiki kinasaidia kufahamu karama apewazo mhubiri wa injili na Roho mtakatifu na kuzitumia vema kadri roho ili upate kuvuna wengi wenye dhambi waliopotea na kuwarejeza kwa mungu au bwana Yesu.

Ktk hii kanisa ilizoeleka kufanywa na wainjilisti labda pengine wainjilisti kutojifahamu nafasi yao ndani ya kanisa au uchache wa wahubiri waliotwa na kwa kazi ya kuhubiri injili.

Mtume Paul hutumia huduma mhubiri kuhubiri injili kwa wenye dhambi waokoke hakusema yeye ni

## SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

**Mhubiri** ni mtumishi wa Yesu anayewahubiria wenye dhambi waokoke.Hupelekwa na roho mtakatifu wanapokaa ktk ushirika mzuri na roho mtakatifu kwa njia ya maombi au kwa kutii agizo la yesu la kuhubiri alilowatuma mitume . Yeye naye hushiriki ktk kuliongeza kanisa kwa wenye dhambi wanapookoka. Tofauti yeye haanzishi kanisa bali huliongeza kanisa bali mitume huanzisha na kuiliongeza kanisha.**Mhubiri (agano jipya)**kusudi ni moja yesu humtumia kuokoa waliopotea ktk dhambi isipokuwa una kibali cha kwenda taifa hadi taifa dunia nzima kuhubiri injili ya bwana yesu. Mfano wa mtumishi wa yesu ni mtume Paulo alikuwa na huduma ya mhubiri ndani yake kwa mataifa.

**Mhubiri wa kimataifa** kusudi ni moja yesu humtumia kuokoa waliopotea ktk dhambi isipokuwa una kibali cha kwenda taifa hadi taifa dunia nzima kuhubiri injili ya bwana yesu kwa watu wanaofanyakazi ktk nyanya mbalimbali za kimataifa kama mashule ya kimataifa, waandishi na watangaji wa habari za kimataifa, wanamichezo wa kimataifa mfano mpira na riadha na wafanyabiashara wa kimataifa na wa mashirika ya kimataifa kama ndege. Neno la mungu alinipa huduma hiyo mwaka 2003 nilipookoka mimi lameck lister.(jina hili la mhubiri wa kimataifa kwa kumpokea Yesu mimi ni **agano jipya** la damu ya yesu)

**Tahadhari: mhubiri(agano la kale)** jina la mfalme aliyetawala mji wa jerusalemu alikuwa na hekima alitumia kufundisha watu maarifa. Kwa leo Ukiokoka yesu akikupa Hekima ufundishe kanisa lake maarifa huduma yako ungeliitwa mwalimu wa maarifa kwa kanisa. Ukibatizwa ungeliweza kuchagua jina kama hili la mhubiri au Paulo au Christopher au lile Roho akushudia.

## SURA YA PILI

WITO

Niliokokoka mwaka 2003 nikiwa kidato cha tatu shule ya sekondari kibaha umri wangu ukiwa miaka 17.

Haya ndiyo yaliyojitokeza nilipokuwa namkiri yesu kama bwana na mwokozi kwa kuongozwa sala ya kuokoka. Mbali na kipengele cha toba kwa damu ya Yesu kulikuwa na kipengele cha kumkaribisha yesu na roho mtakatifu waingie moyoni. Macho yangu ya rohoni yalifumbuka nikiwa sijafumba macho ya damu na nyama waziwazi nilimwona mfano wa mwana wa mungu mwenye nuru kuanzia kichwani mpaka miguuni ifunikangozi yote ya mwili na viungo vyake ambavyo si rahisi kuviona. Nikaona akaingia ndani yangu saa hiyo hiyo nikabadilidilishwa ktk roho mbinguni roho ghafla nikasiki roho ndani yangu inacheka nikasema kimoyo moyo ni nani huyu anacheka lakini ktk uso wa damu na nyama sicheki? Ndipo yakathibitika maneno ya maandiko mtakatifu yasemayo:

**“Mbele zake Mungu zipo furaha”()**

Roho yangu iliyozaliwa ilipokelewa na kusimama mbele za mungu mbinguni Baba wa bwana Yesu. Ghafla ile roho ilizidi kucheka kucheka kinywa kikafunguka nikikaanza kucheka na machozi ya furaha yakitoka kama maji uso wangu ulibadilika ktk roho kutiwa nuru kila nikifunga kinywa nasikia ndani yangu kunacheka kimoyo nasema mbona hakuna la kunichekesha kinywa kinafunguka na kuanza kucheka na tukio hilo lilijirudia mara kadhaa. Baadaye nilifahamu kuwa ni upako mojawapo wa ya karama ni hekima;

## SURA YA THELATHINI NA TANO

KUMWONA MUNGU

Kwa nini mungu ajifunue kwa utukufu huo kwangu ? Nafikiri sababu ni hii; siku moja nikiwa ktk kazi ya kuhubiri injili nilikutana kijana mmoja niliyemhuabiri injili ila baadaye alileta hoja nje ya mahubiri ila iliyo ndani ya biblia. Swali lake ni hili mungu anaononekana? Alihoji swali gumu kwa wanadamu wengi wenye dhambi ila sio kwa Yesu amewajibu wanadamu wenye dhambi **Math 8: 5**

**“Heri wenye Moyo safi; maana watamwona Mungu”.**

Nami nilimjibu vivyo hivyo lakini aliendelea kunihoji na kuipinga kweli akifikiri moyoni mwake nimedanganya na haiwezekani akikwepa yale mahubiri ya kuokoka niliyomhubiri.

Bwana aliithitisha neno lake kwa kunitokea na kunionesha umbo lake lililo mfano wa mwana wa mungu bila haki ya kuona mwili wa damu na nyama ni “upako”

- uvumi wa upepo wa pentekoste ulikuwa unavuma kutoka kwa yule mfano wa Mwana wa mungu ndiye Mungu kama alivyoshuhudiwa na malaika wakiwa ktk vazi kama la ganda la nje la zabibu (blue + nyeusi);.

## SURA YA THELATHINI NA NNE

KUMWONA MUNGU

Ilikuwa kati ya mwaka 2009 –2014 Nipo chuo nimepanga TIP –TOP siku hiyo nikuwa nimepumzika ktk kitanda changu na nimeweka net majira ya mchana au alasiri dirisha na mlango vikiwa wazi macho yangu yakikazia dirisha nilisihi jambo nisiloliona ghafla nilichukuliwa na usingizi hata dakika tatu hazikupita niliamshwa na ugeni chumbani wa malaika aliyeingia kupitia mlango Roho mtakatifu ndani yangu akamshudia ni malaika.Mwili wangu ukiwa dhaifu nilisihi jambo nyuma yangu intake kugeuza shingo nikakutana na nguvu kubwa ya mungu/upako au uvumi wapentekonte nilipotazama nikaona mfano wa mwana wa mungu mara yule mara yule malaika aliyeungwa ktk ushirika na moyo wangu kuwa yule mungu. Huku nikiwa nausilizia ule upako uliokuwa nguvu nyingi wenye pumzi Imani ikaumbika ktk roho yangu ikisema “akiingia ndani yangu kila udhaifu utaondoka” nikiendelea kumtazama yule mwana wa mungu roho yake isema roho yangu kwa moyo huo udhaifu ulilonalo nitakuponya sikufahamu anazungumzia tatizo gani? Maono ya wazi-wazi yakaisha.Maandiko ya hayajatanguka hatukuona mwili wa damu na nyama kama nabii Musa(Kisogo)

## SURA YA TATU

WITO

Imeandikwa mahali Fulani hekima **“Hekima inalia…”().** Tena imeandikwa ;

**“Ni nani aliye kama mwenye hekima; Naye ni nani ajuaye kufasiri neno? Hekima ya mtu humng'ariza uso wake, Na ugumu wa uso wake hubadilika. ”**
**(mhubiri 8:1)**

Ndipo yule aliyeniongoza sala ya kuokoka akaniambia baada kujazwa roho mtakatifu nimshukuru mungu kwa kusema asante kwa kurudia rudia kwa haraka sana nitapokea karama ya kunena kwa lugha kama ilivyoandikwa ktk **marko 16:16** kufumba na kufumbua lugha yangu ikabadilishwa nikaanza kunena kwa lugha za malaika nikapokea hiyo karama.
Kisha akaniambia wewe sasa ni mwana mbele za mungu omba lolote utapewa, nikaomba peni tulikuwa kwenye maeneo karibu na kiwanja cha basket cha shule tukatoka nafika bwenini mtu mmoja akajitokeza na kunipa pesa bila kumwomba nikataka kumuuliza ya nini ? Ghafla roho mt. akanikumbusha ni ya peni ilikuwa shs. 100 sawasawa na bei ya peni kama nilivyoomba kweli mungu alithibitisha mimi ni mwana mbele zake. Ushirika kati yangu na mungu.
Yesu alinitendea kama yohana mbatizaji alivyosema ndiye atayebatiza kwa roho mt. wale watubuo kwa jina lake **(marko 1: 8)**

# SURA YA NNE

WITO

Siku ile ile usiku nikiwa nimelala nikapata maono; nilionyeshwa nimeketi na mfano wa mwana wa mungu mahali pa juu sana kulikuwa nuru nashudiwa na roho mtakatifu ghafla nikaondolewa ktk sehemu niliyokaa na kupekwa sehemu yenye giza zito nilikuwa nahangaika nimefumbua macho sioni mikono nahangaika nikiwa nimekata tamaa sina matumaini ya kutoka ktk giza nikaamka na kufadhaika.

Siku ya jumapili nilikwenda kanisani bado nilikuwa mkatoliki sijaenda ktk makanisa au huduma za watu waliokoka ile naingia kanisani ibada inaanza tu upako ulio ndani yangu ukaanza kusumbua kwa namna ambayo ulitaka nitoke nje nikatii na kurudi shule nikafika kiwanja cha mpira cha shule nikapumzika karibu na mti wa mpera nikalala chali kuangalia mbingu.

Neno la mungu ndani yangu likaanza kusema toka ndani yangu limeejaa neema ya uaminisho sauti ya msusumo na pumzi ya uzima kama ya uvumi wa upepo wa pentekoste na kushudiwa na roho mtakatifu limejaa maisha yenye uzima kila kitu kilitiishwa roho,mwili, fikra,mawazo tuli kulikuwa amani na kutumia kinywa changu kusema:

- Utakuwa mhubiri wa kimataifa
- Nitakuponya harufu ya jasho la kwapa
- Utajaribiwa sana
- Huna utayari

# SURA YA THELATHINI NA TATU

UPONYAJI WA HARUFU YA JASHO KWAPA

Ktk sura ya nne ; Wito, mojawapo ya ahadi uponyaji wa jasho kutoka kwa Neno la Mungu alionipasha habari kwa Roho mtakatifu. Bwana akalithibitisha neno lake kwa kuniponya kati ya 2013 – 2022. Yesu ni mponyaji na mwaminifu ktk ahadi zake .Ukweli uponyaji ambao kabla sijaokoka, nilikuwa sijawahii kufikiri kama ingeliwezekana nilipookoka 2003 Bwana alinishangaza kwa ile ahadi kuniponya. Tangu miaka hiyo nilidumu ktk kuuomba uponyaji mbele za Baba wa mbinguni, kujiwekea mikono sehemu za kwapa na kupako ulikuwa umekaa sehemu zote za mwilli niwekea mikono wengine walikuwa wanaponywa nilijitahadi nilipoona hayo kwa sehemu yangu hata kumhoji mungu ktk maombi na kuendelea kujiwekea mikono.sehemu za kwapani.Nilibaki na usafi wa kawaida baada kuona kodrai, protector, protex hazikunifaa mara kadhaa nilikuwa naoga ila bila kuzitumia kwa sababu ya mainzi. Bwana akilithibitisha neno lake kwa ile ishara ya kuniponya.

**“Bwana hulituma neno kuponya”** kwa sisi tuliokoka bwana ni Yesu.Hivyo Yesu alilituma neno lake mwaka 2003 kwangu kuniponya. Hakuna linaloshindikana kwa Yesu. Mungu Baba wa Yesu na Yesu Asante.

## SURA YA THELATHINI NA MBILI

UPONYAJI WA HARUFU YA JASHO KWAPA

Mwaka 2001—2003 kabla sijaokoka nipo o'level kibaha secondary mazingira shule yalikuwa yanaruhusu kuwa safi Ruvu ipo karibu maji yanapatikana shule.

Ukweli nilijitahidi kuwa msafi kwa kuutafiti ule ugonjwa, kwanza nilioga bila sababu ulikuwa harufu mbaya iko pale , kwa sabuni za kawaida (si za kuzuia) inzi hutua kwenye kwapa kidogo na harufu jasho huwa mbaya, kwa sabuni za kuzuia harufu mbaya ya Jasho kama Protex, Detol nazo hakufaa hurufi mbaya jasho na mainzi hutua kwenye maeneo karibu na kwapa kufuata ile harufu. Kodrai haikufaa kabisa. Hilo jasho lilinifanya nikose heshima ktk jamii yaani udharaurike. Shetani alilitumia hilo kunitesa kimawazo hata kifikra nakujiona ulimwenguni mpitaji .

Mwaka 2003 wakati naokoka sikuwa Imani hata ya kuponywa nilifikiri ningebaki na ile harufu ya jasho sikuzote.

**"Mambo ambayo jicho halikuyaona sikio halikuyasikia wala hayakuwemo ktk moyo wa mwanadamu mambo ambayo mungu aliwaandalia wampendao"**

**(1kor 2:9)**

## SURA YA TANO

WITO

- Usiite shetani (usikufuru roho mtakatifu)
- Utaingia mbinguni (nilichofahamu ningeliingia mbinguni (mkao) baada ya kufa nikiwa nimemaliza kutumikia mungu)

Tafsiri ya kila neno la mungu la ahadi hapo juu imo ktk biblia. Sikuwa na shaka ile sauti iliyosema name nilifahamu ni ya mungu. Baadaye nilibadili dhehebu toka ukatoliki hadi huduma ya efatha ambalo kwa sasa ni kanisa ambaye mwanzilishi wake alitumwa na Yesu. Kuondoka kwangu ni amri, ni vizuri ukiokoka kuhamia kanisa au huduma ambayo utapata mafundisho ya kukua kiroho na kutambua nafasi yako ndani ya kanisa. Baada ya kuokoka usikae mahali ambapo utadumaa kiroho.

Mhubiri ana neema ya kutumiwa na yesu na kuokoa wenye dhambi wengi sana yaani wenye dhambi wengi wataokoka ukihubiri injili ya yesu.

NB: mhubiri na mwinjilisti wana tofauti.unafahamu kuna jambo hata wewe linaweza kukusumbua ukiwa ni msomji wa biblia pia ukitazama wahubiri na wainjilisti waliopita unaweza sema

| Mhubiri | Mwinjilisti |
|---|---|
| -Anahubiri injili kwa wenye dhambi wapate kuokoka.<br>-Amejaa hekima, miujiza, uponyaji, Amri ya kutoa pepo | - Atangaza injili (wokovu ) kwa kanisa(watu waliokoka) moja ya hudumuma kuu tano za kanisa.<br>-Amejaa uweza, miujiza, uponyaji, Amri ya kutoa pepo na nguvu za giza |

## SURA YA SITA

HEKIMA

Ilikuwa siku ya Jumapili nilikuwa ibadani ktk kanisa la efatha nikasikia sauti ndani ya roho yangu ikiwa na msusumo (ikishudiwa na roho mt. kama ile ya mwanzo ikisema "hekima") roho mtakatifu alisema hayo mojawapo zawadi aliyonipa ni hekima mbali karama ya kunena kwa lugha na zinginezo.

Ukweli ukipewa hekima unahitaji kusoma biblia kila siku ukitakutembea ktk uwepo wa mungu na yesu ili kutimiliza kusudi la mungu kwako kwa amani.

Ukiwa mhubiri si kusoma na kwenda kuhubiri kadri roho mtakatifu atakavyokuongoza ukifuata agizo la Yesu kama unaweza kila siku. Utaitumia hekima kuwahubiri watu habari za yesu mfufuka ikiwa unahuduma moja tu ya mhubiri ila kama upo na huduma zaidi ya moja kama mtume Paulo pengine kwa kutamkiwa yesu au roho mtakatifu ualimu na mhubiri zikiwa pamoja ukipewa hekima utumie kwa ualimu wa kanisa si kuhubiri kama mtume Paulo alivyotenda. Ila ukiwa huduma ya mhubiri peke yake uliyoipata kwa kutamkiwa yesu au roho mtakatifu ukapewa hekima itumie kwa kuhubiri kama mhubiri Filipo

Aliyejaa roho ya hekima kabla kuchaguliwa ktk matendo ya mitume kutatua mgogoro wa wajane wa kiyunani na kiebrania pia alijaa miujiza mingi, uponyaji na amri ya kutoa pepo.

Jiepushe na kufundisha au kuonya ikiwa upewa hekima na una huduma moja ya mhubiri ndani yako usiikosee neema ya mungu itutumie kuhubiri injili. Huduma yako itakuwa mafanikio kwa kuzaa matunda yadumuyo yaani waokokao wasioicha Imani.

## SURA YA THELATHINI NA MOJA

UPONYAJI WA HARUFU YA JASHO KWAPA

Mwaka 1999 nilipatwa na tatizo baya sana harufu mbaya sana ya jasho la kwapa kupita kiasi nikiwa darasa la sita shule ya msingi Kawawa. Tangu nizaliwe mwaka 1986 hadi mwaka 1998 sikuwa nanuka harufu mbaya ya jasho la kwapa.

Chanzo cha tatizo haikuwa inatokana na tabia za uchafu wa mwili wa kutokuoga kama wengi wasemavyo na wafikilivyo ilitokana **Neno** lilotamkwa na Baba yangu Lister Daudi akiwa bado hajaokoka. Siku hiyo nilikuwa nimetoka kuoga mama alikuwa akinisifu mbele za baba kuwa ni msafi baba asema **"utanuka jasho mpaka mataifa yatakukimbia"** siku chache baadaye nilianza kuna harufu mbaya ya jasho la kwapa.Nilijitahidi kuwa msafi lakini haliiliendelea kuwa vilevile.

Hatua za utatuzi wa tatizo la jasho; siku moja nikiwa darasani la sita Mwalimu sika akasema ukitaka kuondoka na harufi mbaya ya jasho la kwapa ukiamka asubuhi chukua maji ya kwenye ukoko wa ugali mlikulia jana usiku na upake ktk kwapa kisha ukaoge baada ya siku kadhaa itaacha kunuka. Nilifuata yale maelekezo kwa siku kadhaa bila mafanikio.Baadaye nikayaacha.

## SURA YA THELATHINI

MHUBIRI WA KIMATAIFA

Neno la mungu akikuita kuwa mhubiri wa kimataifa atakupa upako mfuate Yesu jinsi ya kupokea upako na upokelewe na Yesu na Baba yake ukiupata funga kaa ktk maombi ya kuombea watu waokoke,nenda kawahubirie watu waokoke pia usiache kutafakari biblia kila siku.

Mhubiri wa kimataifa neema yake ni kwa ajili ya kuwahubiri wenye dhambi wanaofanya kazi kimataifa waokoke kama wafanyakazi ktk mashule ya kimataifa, mashirika ya kimataifa kama ya ndege (marubani),Michezo kama mpira,waandishi na watangazaji wa habari za kimataifa, Mahakama na vyuo vya kimataifa. Ukiwa chini ya mitume unaweza kutumiwa na Yesu kuwahubiria injili hata wenye dhambi wasiofanya kazi kimataifa waokoke kwa sababu upo chini ya agizo la Yesu kwa kitume la kuhubiri.

Ndivyo walivyo wahubiri wa injili wote waliopata utmishi wao kwa kuokoka wanapaswa kutimiliza huduma zao kwa kuwahubiri injili wenye dhambi waokoke karibu kila siku kwa kadri Yesu Bwana wa mavuno na Roho mtakatifu atakavyowapeleka.

## SURA YA SABA

UPONYAJI

Baada ya kuokoka baadaye tulifunga shule nafika nyumbani nilimkuta Jackson mdogo wangu wa kiume ana ugonjwa wa enia (ngiri) na mama ameacha wokovu (maana aliokoka kati ya miaka 1990– 1995) na kubaki na ukatoliki jina mpaka Jackson anazaiwa 2002. Kama ilivyo desturi ya wa mama wakitanzania wasiomulewa mungu alishampeleka mtoto wa waganga wa kienyeji na kumvisha Hirizi mikononi na kiunoni kama ulinzi dhidi ya nguvu za giza.

Akaniomba nimuombee Jackson apone ule ugonjwa wake Roho mungu ndani yangu haikupendezwa na zile hirizi hivyo nilimuoombea kwa kumuwekea mkono mahali pa mwili penye ugonjwa kisha nilikata hirizi zote mbili ya kiunoni na mkoni na kuzichukua na kuchoma moto baadaye nikamkaidhi kwa kuombea ulinzi wa mungu na kumwambia mungu huyu ni wako umemuumbe umpokee kama nabii Samweli. Tangu siku hiyo ugonjwa wake ukawa umeponywa na Mungu Baba wa Bwana Yesu. Nilienda shule tena nikarudi afya yake ilikuwa Njema alikuwa anaendelea vizuri.

Siku moja niliugua malaria mwili ulikuwa wa moto nilihisi baridi na kutetemeka nilikuwa nyumbani mabibo— DSM (Tanzania) na familia yangu majira ya usiku kati ya saa moja usiku na saa nne usiku maana ilikuwa anandaa chakula cha ajabu siku hiyo akili ya kumwambia mama haipo kwamba ninaumwa nikiwa nimekaa kwenye kochi hali naendelea kutetemeka nikawawa nasikia sauti ikinihoji ya mawazo hivi ulivyokuwa hujaokoka hali kama

## SURA YA NANE

UPONYAJI

Hii unafanye? Nilijibu kimoyomoyo ningelienda hospitali ikanisisitizia niombe nikafanya hivyo nikalala kuamka asubuhi nimeponywa malaria; homa (mwili kuwa wa moto kumetoweka) ,kutetemeka hakupo. Kweli Yesu ni Mponyaji.

Niliugua tena malaria kati ya mwaka 2005— 2007 nikiwa kati ya kidato cha tano na sita shule ile ile ya kibaha sekondari maana nilifaulu. Siku hiyo nilikwenda hospitali na kupima ikagundulika malaria nikapewa dawa na kurudi shule nilipofika bwenini nikataka kuchukua dawa nianze dozi nasikia ikiniambia niweke dawa lokani na niende darasani hali bado si nzuri nikatii kufika darasani nikasikiliza vipindi vyote narudi darasani ile malaria imetoweka basi nikachukua dawa na kwenda kutupa nje. Mungu Baba wa Bwana Yesu hachangamani na magonjwa.

Ilikuwa baada ya kumaliza kidato cha sita 2007 nilirudi nyumbani DSM nikawa naishi na kaka zangu moja ya kaka yangu aliugua tumbo la kuhara au kuendesha tangu asubuhi ilikuwa usiku akaniambia anaendesha (tumbo linamuuma mara kwa mara na kwenda kuharisha chooni) nikamwamwambia njoo nikuoombee akakubali nikaweka mkono kwenye tumbo na kumuombea uponyaji kwa jina la Yesu. Akalala vizuri mpaka asubuhi kufika asubuhi akaenda chooni na kuendesha mara moja tu akaondondoka kufika jioni nikamuuliza hali yake akaniambia tangu niende chooni asubuhi sijasumbuliwa tena tumbo la kuendesha. Yesu ni mponyaji.

Siku nyingine nilimkuta kaka yangu John anaumwa jino .

## SURA YA ISHIRINI NA TISA

USHAURI KWA WAHUBIRI

Ukweli yesu akikuita Mhubiri kwa roho mtakatifu hukupa hekima, mamlaka dhidi pepo, uponyaji na miujiza. Karama hizo zote unapaswa kuzitumia kumdhirisha mungu kwa wenye dhambi hata ufike mahali pa kutubu kwa jina la yesu na kubatizwa kwa Roho mtakatifu.

Matumizi ya hizo karama kwa mhubiri aliyeitwa na Yesu mwenye huduma moja ndani yake ya mhubiri wa injili;

- Hekima — kuhubiri injili ya Yesu kwa wenye dhambi wapate kuokoka.
- Uponyaji—kuwaponya waokokao ili kuwaondolea laana ya magonjwa .
- Miujiza— kuwawezesha wenye dhambi(wasioamini) wapate kumwamini Yesu na kuokoka.
- NB: Ukweli hekima inaweza kukuvutia kufundisha kanisa epuka kujiongezea majukuu; Ktk kitabu cha-Mithali 1: 20 –33 tunasoma mfano wa hekima inavyoweza kutumika ktk kuhubiri huyu ni mfalme sulemani mwenye hekima aliyopewa na mungu. Naongea na mtumishi wa yesu mwenye huduma moja tu ya mhubiri wa injili usipote kihuduma na kusudi.

## SURA YA ISHIRINI NA NANE

KUOKOKA

Mwaka 2009 Tulikuwa kwa kwa kazi ya kuvuna ktk kanisa la efatha kitunda Yesu alinitumia kumhubiria dada mmoja aliyekuwa anakaa ktk nyumba iliyokuwa inatazama na kanisa hilo na aliokoka. Huyu alipokea Roho mt kama Yesu tofauti ktk ishara tu Yesu njiwa huyu machozi ya furaha **"Hekima inalia…". (Mithali 8:1)**

Kati ya mwaka 2007— 2009 Yesu alinitumia kumhubiria mdogo wa rafiki yangu Jonathan aitwaye Grace na aliokokoa. Huyu alipokea upendo wa mungu na Mungu Baba wa bwana Yesu alimbariki kwa kumpa elimu, kazi, mume na watoto ktk maisha yake ya wokovu.

Kati ya mwaka 2003— 2005 Niliombea familia yangu iokoke aliokoka Baba na dada zangu wawili Rozi na Rosalina mama aliyekuwa ameacha wokovu alitubu kwa upya na kuanza upya maisha ya wokovu.Kati ya mwaka 2005—2007 Yesu alinitumia kumhubiria Rafiki yangu Sosthenes nnyani tukiwa advance shule ya Kibaha aliokoka ktk mkutano wa mwalimu Christopher Mwakasege.

Mhubiri wa injili(wa taifa,mataifa,kimataifa) hutumiwa na Yesu kwa kusudi kuu la kuwahubiria wenye dhambi waokoke.

## SURA YA TISA

UPONYAJI

Ametumia dawa ya kuondoa maumivu lakini bado maumivu yako pale pale jino linaendelea kuuma nikamwomba nimuombee akakubali alikuwa hajaokoka kama kaka yangu eliste wakati mwingine siyo rahisi kukubali kuombewa. Nikamwekea mikono shavuni mahali penye jino linalouma jino likaacha kuuma maumivu yakatoweka baada ya kutoa mkono nilipomuuliza akasema hasikii tena maumivu hakuendelea kutumia dawa wala kwenda hospitali kung'oa jino. Kweli Yesu ni mponyaji.

Siku moja ilikuwa jumapili nilipitia rafiki (ameokoka) ili twende kanisani nilimkuta amelala hawezi. Nikamshika mkono mwili ulikuwa wa moto (homa) ghafla ukabadilika na kuwa wabaridi. Akainuka na kuniambia naenda kuoga ili twende kanisani nilipomuliza hali yake anasikia vizuri. Nilistaajabu hata mimi kweli nilikuwa sijamuombea. Kweli Yesu ni Mponyaji **.(marko 1: 30-31).**

Lakini huyo rafiki yangu alikuwa mgumba alizaa mtoto mmoja wa kiume hajawahi kupata mtoto tena kila mimba anayobeba ilikuwa inaharibika. Siku moja nikiwa rafiki zangu wa chuo nikiwa ktk chumba chake nafanya kazi za chuo nashuhudiwa roho mtakatifu toka ndani Yesu amesimama juu sio mbali sana na paa la nyumba niliyokaa nikasikia sauti yake ikiongea na moyo wangu kwa msusumo (utukufu) ikizungumzia habari ya yule rafiki wa kike mgumba kuwa amempa mtoto. Haikupita siku nyingi akapata mimba. Akasubiri siku za kuharibika zipite ukweli haikuharibika wala kutoka siku zikapita na kuzidi. Kweli Yesu ni mponyaji.

## SURA YA KUMI

UPONYAJI

Siku moja mtoto wa kaka yangu wa kwanza John alinijilia na kunimbia kichwa kinaamuuma nikamwambia njoo nikuombee akakubali nikaweka mikono kichwani nakaweka mikono kichwani na kumuombea kisha nikatoa nikamuuliza vipi hali yako akasema kichwa kimeacha kumuuma. Yesu ni mponyaji.

Siku moja nilienda hospitali ya Mwananyamala nikaomba kibali cha kuombea wagonjwa wakanipeleka wodi mbili zilizoungana. Kulikuwa na wagonjwa wamelazwa mkono wakuume na wakushoto wazile wodi. Nikapita na kuwawekea mkono kisha nikawaombea uponyaji ila mgonjwa wa mwisho wodi ya pili mkono kuume alikataa nisimuombee nilipomtazama alikuwa jirani dini muislamu umri umekwenda basi nikamwacha sikumuombea nikarudi nyumbani. Kesho nikaenda tena kuwajulia hali wale niliowaombea nikaomba kibali cha kuwaona wanaendeleaje wakaniruhusu nikaingia zile wodi nikakuta hali za afya ni njema wengine wamekaa sio wamelala hali hawawezi nikawauliza kulikoni wasubiri nesi / daktari apite na kuwajazia kadi ya kuruhusuwa kutoka wodini. Nikafika kwa jirani aliyekataa nisimuombee nikakuta kitanda tupu, nikawauliza wagonjwa wa upande wa kushoto ambao hali zao zilikuwa nzuri baada ya kuwaombea jana

Yu wapi jirani yangu mbona kitanda ki tupu? Wakanijibu amefariki jana Usiku. Ilikuwa ni nafasi ya kuponywa kama wenzake alikataa ilikuwa ni nafasi ya kuokoka na kwenda mbinguni alizikataa. Hata Yesu ni Mponyaji Mkuu ni jibu la kifo.

## SURA YA ISHIRINI NA SABA

MALAIKA

Maono ya malaika walionifungua pingu zilizo ktk miguu yangu . Ilikuwa siku ya jumapili nilikuwa ibada efatha Mwenge DSM wakati ibada inaendelea tukiwa tumesimama bahati nzuri siku hiyo nilikaa viti vya karibu kidogo na mbele si kawaida yangu mara nyingi hukaa viti vya nyuma nguvu ya mungu ilishuka nusura nianguke nikiwa sijafumba macho ya mwili ghafla macho ya rohoni yakafumbuka Nikaona malaika wawili wakiwa wamezungukwa nuru nzuri sana yenye rangi isiyoumiza macho kama ya njano na mavazi marefu kama kanzu yenye mfano wa weupe wa kati waliniangazia nuru walikuwa na umbo la mwana wa mungu kama Yesu la jinsi ya mwili rangi ya ngozi ni nzuri na zina utukufu kupita za wazungu. Wakati huo huo nikaona ktk miguu yangu nimefungwa pingu wale malaika kunitoa zile Pingu. Huo ndiyo mwisho mwa hayo maono . Yesu alichonitendea ni kunifungua kwa kutumia wale malaika

**(Efatha—funguka marko 7 : 34).**

Yesu akikuita mhubiri wa injili hufahamu malaika hutumiwa na Yesu kukuongoza kwa mtu au watu wa kuwahubiria injili yake. **Matendo 8 :26 –35**

## SURA YA ISHIRINI NA SITA

KUMWONA YESU

Kati Ya mwaka 2004 –2007 Nikiwa sekondari Kibaha Advance Nlikuwa chumba kikubwa chenye vichumba vitatu  mara nilisikia sauti kama ya mtu aliaye nilimtafuta ktk vyumba vyote nisimwone  nilitoka nje ili nimwone ghafla nikasukumwa niangalie juu ya dunia nikaona ktk roho na macho ya damu na nyamba nikiwa sijayafumba

Mbingu zimefunga na mlango wa mbinguni umefunguliwa Yesu ametoka amesimama juu ya anga ndani nashudia na Roho mtakatifu kuwa ni Yesu akasema neno moja tu **Biblia** lile neno liliingia mpaka ndani ya moyo wangu maono yale yakaisha na ile sauti iliayo sikuisikia Tena. Nilifahamu baadaye ni ya roho Mtakatifu. Huu ni Ushuhuda Yesu amefufuka yupo hai hadi leo

Mhubiri wa injili uwe wa kitaifa,wa mataifa au wa kimataifa ushuhuda wa kumwona yesu ukutie nguvu ya kuamini na kudhidi kuhubiri ile habari njema kwa wenye dhambi  ya kuwa yesu alisulubiwa kwa ajili ya dhambi za watu na siku ya tatu alifufuka awape maisha mapya ndani yake wale wote wamwaminio.

**Math 5: 8 "Heri wenye moyo safi maana hao watamwona mungua"**

## SURA YA KUMI NA MOJA

UPONYAJI

Ktk kile kikundi chetu cha maombi alikuja mama mmoja aliyeokoka na kuacha wokovu mwenye mtoto aitwaye jack. Alishiriki nasi kwenye maombi ndipo yesu alipotutumia kumresha kwenye wokovu. Ukweli alikuwa na tatizo ktk mwili wake lililomtesa sana (fimbo : Zab 23: 4)  aliendа mara kadhaa hospitali kupima wasione ugonjwa na kanisani alikuawa ameacha kwenda siku nyingi tu.

Nikamsomea maandiko matakatifu  ya kwenye biblia **ZAB: 103:23  "Akusamehe maovu yako yote, akuponya magonjwa yako   Yote";**

Kisha nikamwambia atubu arejee kanisa sitakuwekea mkono kukuombea katii kwanza rudi ktk ushikirika na wenzako wa kanisani  na mungu atakuponya. Akafanya hivyo siku iliyofuata akaungana na wenzake wa kanisani  kwa ibada baadaye alirudi nyumbani bado akiwa na mateso yasiyoeleweka ktk mwili alijikuta anasukumwa kusoma biblia achukua kuifungua akakutana na andiko lenye pumzi ya mungu ya uponyaji kila akitaka kulivuka anarudishwa hapo hapo mara mateso yake yakatoweka baada ya kulisoma. Siku nyingine akaungana nasi kwenye kikundi cha maombi  na kutushuhudia kweli Yesu ni mponyaji.

Kaka yangu John Lister alikuwa anaumwa tumbo  Akaniambia tumbo linamuuma. Nikaweka mkono juu ya tumbo na kumwobea kisha nikatoa. Nilipomuuliza hali yake akasema tumbo limeacha kuuma.Yesu ni mponyaji.

## SURA YA KUMI NA MBILI

UPONYAJI

Maono ya uponyaji nilioona kati ya mwaka 2003—2005 kwa mtu ambaye mguu wake ulikuwa umepinda kwenye sehemu ya kukanyagia(foot) na mfupi tangu kuzaliwa kuliko mwingine ambao upo sawa yaani hauna tatizo.Nilikuwa nimelala usiku ktk maono nikaonyeshwa mtu ambaye nilipotaka kumwangalia nilijikuta nimechumaa chini na kumwekea juu ya ule mguu ambao upo nusu wayo ambayo wayo yake haijakamilika na kumwobea ule mguu wenye nusu wayo ukaanza kuongeza na kufikia wayo kamili. Yesu ni Mponyaji.

Mwaka 2003 mwezi 10 kusanyiko Precious Center tulikuwa ktk ibada na siku hiyo watumishi walio chini ya Mtume na Nabii J.E Mwingira walikuwa wanapitia kuombea wagonjwa ; kuna mtu alikaa karibu nami sehemu ya wagonjwa nimuuliza jirani huyu anatatizo gani kumjulia hali akaniambia hasikii maana yake ni kiziwi nikamwambia utasikia palepale yule mtu akapokea uponyaji. Yesu ni mponyaji.Yesu ni Mponyaji kweli ila ana mamlaka kuzuia ugonjwa au magonjwa kabla ya kutokea ikiwa roho atakupasha habari ukaingia kwenye maombi ya kuomba uepushwe mtu uliyeokoka. Mwaka 2004 nilikuwa kidato cha nne ; ilikuwa kawaida kwa magonjwa kuwapata wanafunzi siku za mitihani ya taifa ya kidato cha pili, nne na sita kama macho, malaria wakati mwingine hushindwa kufanya mitihani. Nimshirikisha kijana aliyeokoka anaitwa gaspa mchaki kuhusu hilo swala. Tukakubaliana kufunga siku tatu ili wote tufanye mtihani wakidato cha nne 2004 tukiwa salama. Yesu mponyaji akatutendea hivyo. Amen

## SURA YA ISHIRINI NA TANO

ELIMU

Kati ya mwaka 2003 –2005 nilisikia tena sauti ya Roho mtakatifu ndani yangu ikinipasha habari juu ya daraja la kwanza ningelipata ktk matokeo yangu ya kidato cha nne kabla ya kufanya mtihani wa taifa wa mwaka 2004.

Ukweli yesu alinipa Division one na nilipata A ktk kila somo l a combination (PCM). Yesu aweza kukufanikisha ktk Elimu ya chekechea hadi chuo kikuu inayotokana na Hekima ya Kibinadamu.

Yule rafiki yangu aitwaye Jonathan Mwakajinga alikuwa na dada yake Grace Mwakajinga alikuwa amemaliza kidato cha nne matokeo yalitoka amefeli.Aliponiambia kuwa amefeli kiasi hicho nilishangaa nilimuuliza masomo yale aliyokuwa anafanya vizuri yote alipata grade ya chini. Nililienda mbele za mungu na kumwombea Grace Mungu aingilie kati matokeo yake . Baadaye Baraza la mtihani likatangaza kurudia kusahisha mitihani ya kidato cha nne. Iliporudia Grace alifaulu na kwenda kusomea ualimu. Kweli Yesu aweza kukufanikisha ktk Elimu.Mhubiri wa injili unapaswa kujifunza kubariki waokokao kabla ya kuwakabidhi kwa mchungaji ,mtume,mwalimu,nabii na Mwinjilisti.

# SURA YA ISHIRINI NA NNE

ELIMU

shetani aweza kumtumia kuharibu Baraka zako au kukuchelewesha ktk kazi ya mungu. Hii ndio maana ya yale maono ya kuonyeshwa nyoka anataka kunigonga kisigino baada ya kutoka kanisani.

Mwaka 2010 nilikuwa nipo chuo kikuu mwaka wa kwanza nilisumbuliwa HELSB ijapokuwa nilipata mkopo 100%

Sikuletewa ada ya chuo wala pesa ya chakula nilifuatilia kwa muda wote wa semester sikuweza kupewa mitihani seminister ilikuwa imekaribia kwa kawaida hurusiwi kufanya mitihani kama hujalipa ada hata nusu.

Basi niliingia gotini na kumweleza kuhusu yule mtu anayesughulikia swala langu kule HELSB afanyeje? Kama kuna uzembe huyo mtu ampumzishe kazi hata mwezi moja na nyumbani pawe pakavu kama alivyonisumbua mimi semester nzima na akove pesa ya kula yeye na familia yake. Kesho yake nilienda HELSB niliingia ofisini nilikutana anayeshuhulikia swala langu lakini cha ajabu palepale akalishughulikia kwa haraka akaniambia nenda kila kitu utakuta tayari nirudi chuo nilikutana na invoince imefika hivyo nilikuwa nimeruhusiwa kuingia kwenye bank. Yesu ni mtetezi ktk elimu.

# SURA YA KUMI NA TATU

UPONYAJI

Siku moja nilitembelea familia ya rafiki yangu anayeitwa Yona kama Yesu naye alikuwa na rafiki aitwaye lazaro familia nzima alikuwa anaipenda; Nilimkuta dada mmoja aitwaye lusubilo ametoka hospitali amepewa dozi nzito ya Pressure(B.P) akiwa amelala kwenye mkeka hoi nikamuuliza kulikoni? Akanieleza anaumwa pressure. Nikakumuka mtume na Nabii J.E Mwingira

Ukimuona mtu anaumwa pressure ujue ana uchungu unaotokana na dhambi ya kutosamehe. Nikamuuliza kuna mtu moyoni hujamsamehe amekutenda vibaya umeshikikilia kwa lile alilotenda hutamsamehe ujue huyo ndiyo chanzo cha tatizo ukisamehe utapona. Nikaondoka akafanya kama nilivyosema jioni kesho hali yake ikawa nzuri hakuendelea kumeza dawa nilipokutana naye nikamuuliza mbona hali yako ni nzuri ni kweli kuna lilimuumiza moyoni sasa amesamehe ndiyo maana hali ni nzuri na dawa ameacha kutumia. Yesu ni mponyaji yeye ni kimbilio kwa walio hawawezi.

Nilichofahamu kwa shuhuda hizi chache za uponyanji kwa hekima nilifahamu kuwa nilipewa na roho mtakatifu karama ya uponyaji hayo ni sehemu ya ule upako niliopokea siku naokoka (Neno la mungu ,nuru) ikiwemo na hekima kama ulivyosoma ktk sura ya sita.

Na mimi mhubiri wa kimataifa Roho mtakatifu alinipa Hekima na Karama ya uponyaji Kwa ajili ya kuwahubiri wenye dhambi Yesu mfufuka na kuwaponya waokokao magonjwa yao(Laana zao).

## SURA YA KUMI NA NNE

MIUJIZA

Siku moja nimerudi nyumbani (mabibo - DSM) nilikuwa nataka niingie chumbani mlango ulikuwa umefungwa na kufuli nilifikiri nina funguo nikajisachi mifuko yote sukuwa nayo kumbe alikuwa nayo mama. Nikaivuta ile kufuli kwa mkono bila funguo haikufunguka mara kadhaa nikaacha baadaye kidogo nikajikuta naikazia ile kufuli macho muda mchache na kuivuta kama mwanzo mara kufuli ikafunguka bila kutumia funguo nikastaajabu na kuingia chumbani ukweli kufuli haikuwa mbovu baadaye kidogo mama akarudi nyumbani nilimuliza kuhusu funguo kama anao akajibu ninao. Nilibaki nimestaajabu Yesu ni wa Miujiza.

Nilipokuwa nimemaliza kidato sita 2007 nilirudi nyumbani kwa kaka zangu ; Tandale — DSM na kuishi nao baadaye nilikuta na marafiki zangu wawili waliokoka moja alikuwa anasali TAG na mwingine EAGT tuliunda kikundi cha maombi. Siku moja rafiki yangu wa EAGT John chrispin alituambia tumuombee mama wa rafiki yake amevamiwa na majambazi na kupigwa risasi amelazwa hospitali madaktari wamejaribu kumfanyia upasuaji ili kutoa risasi zilizoingia kwenye mifupa ilishindikana. Basi tukamwombea mbele za baba wa mbinguni afanye maajabu yake. Kesho jioni chrispin akaja kwenye maombi nikamuuliza hali ya mgonjwa akasema asubuhi ya leo madaktari walitaka kwa ajili ya upasuaji tena walikuta risasi zimetoka zenyewe kwenye mifupa. Kweli Yesu ni wa miujiza.

## SURA YA ISHIRINI NA TATU

MKE

Kati ya mwaka 2008—2013 Nikiwa nawahubiria watu wenye dhambi waokoke nikikutana na mtu mwenye uhitaji wa kuombewa namuombea . Nilikutana na mama mmoja aitwaye Pendo aliyenitambulisha kuwa ameokoka. Yule mama alijitambulisha yeye ni mke na ameniona ktk majaribu mbalimbali ya wanawake.

Kabla ya hapo sikuwa na tatizo hilo mpaka Maono niliyopata kati ya mwaka 2007 — 2009 usiku nikiwa nikiwa nimelala “ nilijiona natoka Efatha kanisani Mwenge DSM baada ya Ibada ya kuisha, nimetoka getini narudi nyumbani ghafla nikahisi kuna kitu kinanifukuza kugeuka nyoka mrefu mkubwa kama chatu alikuwa ananikimiza akitaka anigonge kisigino” maono yakaishia hapo. Kuanzia hapo nilipata aina hiyo ya majaribu ila siku tunakutana naye nilikuwa nimeshinda majaribu hayo yalikuwa yamepungua . Shetani alimdanganya baadaye Nilisikia sauti ndani ya roho yangu ikisema nimwite **“Rafiki”** hakuwa mke bali rafiki.Mhubiri yeyote uwe wa kimataifa au wa mataifa jiepushe na rafiki utayekutana naye njiani ktk kazi ya mungu ya kuhubiri injili usifanye naye uzinzi/uasherati.

## SURA YA ISHIRINI NA MBILI

MKE

Kati ya mwaka 2003 –2005 Ndiyo Nimetoka kuokoka muda mrefu Baba wa Yesu alikusudia kunibariki Kwa kunipasha habari juu ya mke. Nilikuwa bado niko kwa Baba na mama yangu Mabibo—DSM(Tanzania). Mama alinituma dukani nikiwa naelekea dukani niasikia sauti ndani yangu yenye utukufu wa msusumo kama ile niliyoisikia ya wito siku chache baada ya kuokoka ikaongea maneno mawili "Mke Ester" moyoni mwangu nikafahamu Mungu anazungumzia ester jirani yangu aliyeokoka. Baadaye alikuwa amekaa nje ya nyumba nilimtazama nikabaki na mshangao. Mungu akikuambia huyu ni mkeo ikiwezekana kaa baraza naye. Kusahau ni dhambi **"ukikosea kuoa umekosea maisha";**

Wahubiri wote waliopata nafasi ya kuitwa na Neno la Mungu au Yesu kwa kuokoka kwa habari ya mke na ndoa wanapaswa kumfuata Mhubiri Filipo ikiw

A una huduma moja tu ya mhubiri . Ukweli kwa nini Uoe ?watoto wako ni watumishi wa mungu wanaoweza kuwa watabiri kama wa kike ktk kanisa.Kwa habari ya watoto wa kiume ukae ktk maombi kama Bwana Yesu atakupa nao ni nani ktk kanisa?

## SURA YA KUMI NA TANO

MIUJIZA

Siku moja ya jumapili nilimkuta ombaomba nje ya kanisa la Efatha upande wa bank nilikuwa nimetoka nyumbani kuja ibadani nilitoa shs.1000 sikawaida yangu kabla sijaokoka nilikuwa nawapa Tshs.100 au 200. Basi nikaingia ibadani baadaye nikatoka maeneo yale yale mbele bank ya kanisa nikakutana na rafiki yangu sijamwomba pesa nashangaa akaingiza mkono mfukoni na kunipa Tshs.3000 .nilikuwa najiuliza yale maandiko matakatifu ya neno la kinywa cha Yesu ; **"wapeni watu vitu nanyi mtapewa"**

Je utapata mara ngapi? Kupitia muujiza ni mara tatu ndicho nilichojifunza . Yesu ni wa miujiza huthibitisha Neno la kinywa chake kwa Roho mtakatifu. Yesu wangu nilichojifunza kama unampa mtu mwenye uhitaji kitu mfana pesa,nyumba, nguo, gari hurudisha mara tatu.Siku moja nilikuwa sina pesa kabisa ya kula ukweli nilikuwa nahitaji kula mchana nikapiga goti nakuomba Tshs.2000 namaliza maombi tu mlango wa chumba changu nilioufunga kuna mtu alikuwa anagonga hodi nifungue nimtazame ni mgeni yuko mwanae akanipa Tshs. 5000. akaniambishe mwanangu hii kwa mwezi nilipomzama alikuwa atokei eneo lile kabla labda kasikia maombi yangu nikajua huyu ni mungu amejibu sawa na nilivyoomba. Yesu ni wa Miujiza.

Mhubiri wa injili yeyote aliyepelekwa na Yesu ; huweza kutumiwa ktk miujiza na Yesu. Miujiza ni moja ya karama anayoweza kupewa na roho mtakatifu .mfano Mhubiri Filipo **matendo 8:13 ,8:39-40,21:8**

## SURA YA KUMI NA SITA

KUPOZA

Kati ya mwaka 2003— 2005, Baada Yesu kunitumia kumponya mdogo wangu ngiri /enia baba yangu wa jinsi ya mwili aitwaye Lister Daudi akaugua ugonjwa huo. Siku moja akiwa ameshikwa na maumivu yalitokana enia/ngiri kordani moja ilikuwa imeingia sehemu ya kinena kwa hiyo ikabaki kordani moja hata kusogeza mguu shida akasema mwanangu uniombee. Nikaweka mkono juu ya kinena na kumwombea. Yesu alimponya pale pale kordani ikarudi mahali pake zikawa mbili tena maumivu yamekoma ugonjwa haujaondoka. Nini? Yesu amempoza. Bwana asifiwe…!!!. Tangu siku hiyo hajawahi kupata maumivu kama hayo tena.Kati ya mwaka 2011 - 2013 Baba wa rafiki yangu Jonathan Mwakajinga aitwaye Jobu Mwakajinga aliugua kisukari hii ni familia nzima wameokoka. Miguu ilikuwa dhaifu na alikua hawezi kwenda kanisani pia alikuwa anaenda haja ndogo mara kwa mara akinywa maji au soda. Siku moja akaniambia mwanangu una kitu kizuri niombee miguu yangu niweze kwenda kanisani nikafanya hivyo siku chache baadaye akaweza kwenda kanisani Yesu amempoza miguu yake. Nikamuuliza kamuuliza kama kuna lingine linalomtesa akaniambia tatizo la haja ndogo nikamwekea mkono na kumuombea nayo hali iliyomsumbua ikatoweka. Yesu amempoza ila ukimuuliza kisukari bado kipo.Athari za kupoza nilipoteza wote wawili Lister Daudi na Job Mwakajinga. Kwa sababu hiyo sipendi kupoza.Yesu alinitumia kupoza hao ndugu niliowapoteza.Hata Yesu akikuita mhubiri aweza kukutumia. Ukweli alinitumia kupoza mara chache tu ila kuponya mara nyingi .

## SURA YA ISHIRINI NA MOJA

BARAKA

Yesu alinitumia kubariki mama mmoja aliyekuwa mgumba kwa muda mrefu kila akishika mimba zinaharibika alizaa mtoto mmoja wa kiume na alikuwa ameokoka. Nilisikia sauti ya Yesu ikisema nami juu ya yule mama mgumba kuwa amempa mtoto. Haikupita siku chache nilimtembelea alikuwa ana kichefuchefu na kutapika kwenda kupima akaambiwa ana mimba. Yesu anabariki wamwamio hawatayariki.Rafiki yangu mmoja wa kike aliyeokoka alikuwa hana kazi mwenye elimu ya darasa la saba ukweli maisha yake yalikuwa magumu kutokana na kutokuwa kazi. Nilimwombea Yesu ampe kazi . Yesu akampa kazi sawa na elimu yake ilikuwa ya Grocery isiyo ya tatu siyo kama zile kutembeza vitu vya kibiashara ambazo Wenye elimu ya cheti cha darasa la saba wengi huzipata ktk jiji la DSM — Tanzania. Kumbuka mojawapo ya faida ya kazi humpatia mtu chakula. Kweli Yesu anabariki.**Marko:10: 13-16** Yesu anabariki watoto. Wanaozaliwa mara ya pili wanakuwa wana mbele za Baba wa Mbinguni. Yesu aweza kutumia mhubiri wake awaekee mikono kichwani waokokao na kuwabariki mbali na kuwaondolea laana ya magonjwa, mapepo wale waokokao baada kusikia injili.

## SURA YA ISHIRINI

BARAKA

Mtu mwingine tuliyetaka kumbariki ni John Lister mimi na Yesu Wangu. Nilitafakari jinsi anavyonitunza na sehemu ya biashara wateja hamna basi niliamua kumwombea. Wakawa wanajaa  tangu asubuhi hadi jioni ; Baadaye Tulighali kumwombea baada kugundua haja yetu ilikuwa kubariki yeye sio bosi wake wateja wawe wachache au wengi pesa anayolipwa ni ile ile kwa usiku . Nikamwambia kaka wekeza sehemu yako (afungue hata sehemu ya biashara)achana na kuajiliwa ili mungu akubariki. Nilimwambia hivyo maana nilimuona Yesu anataka kumbariki. Kaka yangu angelikuwa tajiri kama angetii kwa kuwekeza maana angembariki kwa muda mfupi na kumtajirisha kwa kumjazia wateja wa kutosha kwenye sehemu yake aliyowekeza asubuhi mpaka jioni kila siku hivyo angeliongezeka ktk kufungua maeneo mengine ya biashara.Mahali Fulani ktk Biblia imeandikwa;

**“Mimi ni mungu nikupaye nguvu za kupata Utajiri “**

Ukweli Yesu  ni wa baraka na utajiri   aweza kukubariki na  kukutajirisha.

## SURA YA KUMI NA SABA

AMRI YA KUTOA PEPO

Kati ya mwaka  2003 - 2005,Tukiwa tunaishi mabibo DSM  na Baba na mama Jackson Lister akiwa amezaliwa nikiwa upako mama akiwa amembeba Jackson kaka wa kwanza John alikuwa ametutembelea amebeba mojawapo ya kanda za video iitwayo Nsuka nguvu za mungu au za roho mtakatifu zilikuwa nyingi ndani yangu macho rohoni yakaona waziwazi pepo (jini) kutoka ktk mkanda wa nsuka akatoka na kumwingia Jackson aliokuwa ameubeba kaka ghafla Jackson akaanza  kulia sana kila mama akimbembeleza anaendelea kulia tu na macho ya damu nyama sijayafumba  pia wakati naliona hilo tukio. Nikainuka kwenda kumtazama mdogo wangu aliekuwa Analia  kumkazia kwenye macho nikamuona pepo hawezi kunitazama anaona aibu  hukwepesha macho na anaendelea kulia. Nikamkemea   kwa jina mara kadhaa na pepo akamwacha mara akanyamaza kimya  na kunitazama ishara za pepo za pepo zilikuwa zimetoweka nikafahamu pepo limeenda. Yesu alinitumia kumtoa pepo Jackson Lister kwa mara ya kwanza tangu niokoke. Yesu ana mamlaka ya kutoa pepo kwa kutumia  watumishi wake. Amri hiyo inaanzia kwa wliokoka, iko juu sana kwa mitume na wahubiri.

## SURA YA KUMI NA NANE

AMRI YA KUTOA PEPO

Siku moja rafiki yangu Jonathan alinichukua mpaka kwa mama mmoja aitwaye mama lucu alikuwa kwenye chumba amekamatwa na pepo aliniita tumwombee. Tukamwekea nguvu ya giza inayomtesa imtoke mara ikamwacha akawa mzima. Yesu alitumia kutoa pamoja na rafiki. Yesu ana mamlaka ya kutoa pepo.

Siku nyingine nilikuwa nimelala usiku utumishi ndani yangu unaendelea kufanya kazi, nikaona maono ; nipo hospitali mbele yangu amelala chali ktk kitanda kama mwenye kuhangaikujifungua ila mtoto anashindwa kutoka nakasikia ya roho mtakatifu ikisema uchawi huku nikishudiwa upo sehemu za siri za yule mama mjamzito ndiyo chanzo cha tatizo lake. Siku nyingine tena akaja rafiki Jonathan kuna mgonjwa amerudishwa hospitali mama mjamzito mwenye mimba ya miezi kumi haoni uchungu . Tukamwombea nguvu inayomzuia asijifungue ikamwachie na ajifungue salama kisha tukamwacha na kuondoka.Yesu ana mamlaka dhidi ya uchawi.

## SURA YA KUMI NA TISA

BARAKA

Kati ya mwaka 2007—2009 Yesu alinitumia kubariki dada lily aliyeokoka mwalimu wa chekechea. Ilikuwaje? Mama alikuwa ametutembelea nyumbani alikaa siku chache kabla ya kuondoka. Siku moja kabla ya kuondoka nilikwenda kufundisha wanafunzi kwenye ile chekechea ya yule mwalimu. Aliniuliza kuhusu nyumbani yupo mama ila anaondoka siku chache baadaye. Alinipa tsh 5000 ya kumpa mama atumie njiani wakati anasafiri.Nilirudi nyumbani na kupatia ile tshs. 5000 mama.Yule dada alikuwa anahitaji eneo kubwa la chekechea maana lile watoto walikuwa wajaa mpaka nje. Nilijisikia furaha nikapiga goti na kumwombea apate eneo kubwa kuliko lile na kumbariki.Ilipita miaka miwili bila kuonana lily nilikuwa chuo. Siku moja natoka chuo nilipita eneo lake la chekechea ya zamani ya llily nikakuta kumefunga nikauliza kahamia wapi? Wakanielekeza nikaenda na kumkuta ana eneo kubwa zaidi na limejaa akaniambia wapo shift mbili kuna wanaoingia asubuhi na wengine mchana. Ndipo Roho mtakatifu alivyonikumbusha yale niliyomuombea lily. Kweli Yesu ni anabariki.